JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
NA UTAWALA BORA

CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)

# MUHTASARI WA UTAFITI (FACT SHEET)

## KAMPASI YA MTWARA

# ATHARI ZA TEKNOLOJIA ZA KISASA ZA OFISI KATIKA KUBADILI MAJUKUMU NA UJUZI WA WAANDISHI WAENDESHA OFISI NCHINI TANZANIA

TIMU YA WATAFITI: Gwamaka C. Sanga | John J. Nzunda | Juslina M. Tuzza

## LENGO KUU LA UTAFITI

Kuchunguza athari za teknolojia za kisasa za ofisi katika kubadili majukumu na ujuzi wa waandishi waendesha ofisi nchini Tanzania.

### Malengo Mahususi ya Utafiti

1. Kuchunguza majukumu na ujuzi wa sasa wa waandishi waendesha ofisi.
2. Kubainisha teknolojia za kisasa za ofisi zinazotumika katika taaluma ya uhazili.
3. Kubaini majukumu na ujuzi wa baadaye unaohitajika katika mazingira ya kazi yanayoendeshwa na teknolojia.

## MBINU ZA UTAFITI

### Muundo wa Utafiti

- Mkabala wa Mseto (Mixed Methods Research Design)

### Washiriki wa Utafiti

Jumla ya washiriki 152 kutoka mikoa minane ya Tanzania:

- Arusha
- Dar es Salaam
- Dodoma
- Kilimanjaro
- Morogoro
- Mtwara
- Mwanza
- Tabora

### Makundi ya Wadau

- Waandishi Waendesha Ofisi
- Wataalamu wa Usimamizi wa Rasilimali Watu
- Wakufunzi wa Uhazili
- Wanafunzi wa Masomo ya Uhazili

### Mbinu za Ukusanyaji Data

- Hojaji (Questionnaires)
- Mahojiano (Interviews)
- Majadiliano ya Vikundi Lengwa (Focus Group Discussions)

## MATOKEO MAKUU YA UTAFITI

### 1 Teknolojia Inabadilisha Majukumu ya Waandishi Waendesha Ofisi

Tafiti hii imebaini teknolojia imepelekea mabadiliko ya Majukumu ya waandishi waendesha ofisi kuwa kama ifuatavyo;

- Usimamizi wa mawasiliano ya kidijitali.
- Uratibu wa mikutano kwa njia ya mtandao.
- Usimamizi wa data na taarifa za kidijitali.
- Usimamizi wa kumbukumbu za kidijitali.
- Kusaidia ushirikiano wa kazi kwa njia ya mtandao.
- Utawala wa ofisi unaotegemea teknolojia.

**Hitimisho:** Majukumu ya jadi ya uhazili yanaendelea kupungua umuhimu huku majukumu ya kidijitali yakiongezeka.

### 2 Teknolojia za Kisasa za Ofisi Zinazotumika

Tafiti hii pia imebaini teknolojia za kisasa zinazotumika kuendeshea ofisi zinajumuisha;

- Cloud Computing.
- Mifumo ya mikutano mtandao.
- Akili Mnemba (Artificial Intelligence - AI).
- Programu za upangaji wa ratiba za kidijitali.
- Mifumo ya mawasiliano na ushirikiano.
- Majukwaa ya ujumbe wa papo kwa papo.
- Mifumo ya usalama wa kibayometriki.
- Zana za kushirikiana na kubadilishana mafaili.

### 3 Ujuzi wa Zamani Unaopungua Umuhimu

- Hatimkato (Shorthand).
- Unukuzi wa maandishi kwa mikono.
- Ujuzi wa kuchapa kwa kutumia mashine za kizamani za kuchapa (manual typewriters)
- Mifumo ya zamani ya kuhifadhi nyaraka.

**Hitimisho:** Ujuzi huu unabadilishwa kwa kasi na mifumo ya kidijitali na teknolojia za kiotomatiki.

### 4 Ujuzi Muhimu Unaohitajika kwa Sasa

Ujuzi huu Unajumuisha;

- Uelewa wa teknolojia za kidijitali.
- Ujuzi wa usimamizi wa data.
- Uelewa wa usalama wa mtandao.
- Ujuzi wa matumizi ya programu za kompyuta.
- Ujuzi wa mawasiliano.
- Uratibu wa miradi.
- Fikra pevu (Critical Thinking).
- Uwezo wa kutatua matatizo.
- Usimamizi wa taarifa.

CHUO CHA UTUMISHI TANZANIA (TPSC)
S.L.P 2574, Dar Es Salaam,
TANZANIA

+255 22 286 0370-5 | info@tpsc.go.tz | https://www.tpsc.go.tz

## CHANGAMOTO KUU ZILIZOBAINIKA

### Changamoto za Kitaaluma
- Uhitaji wa mara kwa mara wa kuongeza na kuboresha ujuzi.
- Upatikanaji mdogo wa mafunzo ya teknolojia za kisasa.
- Ugumu wa kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

### Changamoto za Kitasisi
- Miundombinu duni ya TEHAMA.
- Msaada mdogo wa kiteknolojia.
- Fursa chache za maendeleo ya kitaaluma.

### Wasiwasi wa Maendeleo ya Kazi
- Hofu ya kupoteza ajira kutokana na AI na mifumo ya kiotomatiki.
- Kuongezeka kwa mahitaji ya umahiri wa juu wa kidijitali.

### Changamoto za Mafunzo
- Mitaala iliyopitwa na wakati.
- Kutolingana kati ya mafunzo yanayotolewa na mahitaji ya soko la ajira.

## MAPENDEKEZO MUHIMU

1. Kuanzisha programu za uthibitishaji wa umahiri katika matumizi ya teknolojia za ofisi.
2. Kufafanua upya majukumu na ujuzi wa waandishi waendesha ofisi ili kuendana na AI na teknolojia za kiotomatiki.
3. Kuongeza uwekezaji katika teknolojia za kisasa za ofisi na miundombinu ya kujifunzia.
4. Kuboresha mitaala ya uhazili kwa kujumuisha ujuzi wa kisasa wa kidijitali na kuondoa maudhui yaliyopitwa na wakati.
5. Kuimarisha ufundishaji wa uchapaji kwa kutumia mifumo ya kisasa ya kompyuta na mazingira halisi ya kazi.
6. Kujumuisha mafunzo ya maadili ya matumizi ya AI, usalama wa taarifa, mawasiliano ya kidijitali na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia.
7. Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za mafunzo, waajiri na serikali ili kuhakikisha wahitimu wanakuwa na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

## MUSTAKABALI WA TAALUMA YA UHAZILI

Utafiti umeonesha kuwa taaluma ya uhazili itaendelea kuathiriwa na:

- Akili Mnemba (AI).
- Teknolojia za kiotomatiki.
- Mifumo ya kazi kwa mbali na mseto.
- Uchambuzi mkubwa wa data.
- Uhalisia Pepe (Virtual Reality) na Uhalisia Ulioboreshwa (Augmented Reality).
- Usalama wa mtandao.
- Majukwaa ya ushirikiano wa kidijitali.

## MWELEKEO WA BAADAYE

Waandishi waendesha ofisi wa baadaye wanatarajiwa kuwa wataalamu wa kimkakati wa utawala, usimamizi wa taarifa na uratibu wa shughuli za taasisi badala ya kuwa watendaji wa kazi za kawaida za ukarani.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
NA UTAWALA BORA

# CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)

## MUHTASARI WA UTAFITI (FACT SHEET)

### KAMPASI YA SINGIDA

# TATHMINI YA UFANISI WA UTEKELEZAJI WA MFUMO WA OFISI YA KIELEKTRONIKI (e-Office) KATIKA USIMAMIZI WA TAARIFA KATIKA TAASISI TEULE ZA UMMA NCHINI TANZANIA

TIMU YA WATAFITI: Grayson Msakila • Esther Barnabas • Mathew Kilasi • Abdurahaman Salama • Cecylly Ngudungi
Mhija Ng'wanakilala • Emmanuel Tandika • Lameck Kashaija

## LENGO KUU LA UTAFITI

Kutathmini ufanisi wa utekelezaji wa Mfumo wa Ofisi ya Kielektroniki (e-Office) katika usimamizi wa taarifa katika taasisi teule za umma nchini Tanzania.

### Malengo Mahususi ya Utafiti

1. Kutathmini mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mfumo wa e-Office.
2. Kuchunguza uwezo wa taasisi katika kutekeleza na kusimamia mfumo wa e-Office.
3. Kutathmini mtazamo wa watumishi kuhusu matumizi ya mfumo wa e-Office.
4. Kubaini changamoto zinazoathiri utekelezaji wa mfumo wa e-Office.

## MBINU ZA UTAFITI

### Muundo wa Utafiti

Mkabala Sambamba wa Utafiti wa Mseto (Convergent Parallel Mixed Methods Design)

### Washiriki wa Utafiti

Washiriki 82 kutoka taasisi mbalimbali za umma ambazo ni;

- Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB)
- Tume ya Mipango
- Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
- Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)
- Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)
- Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA)

### Mbinu za Ukusanyaji Data

- Hojaji
- Mahojiano
- Uchunguzi (Observation)

## MATOKEO MAKUU YA UTAFITI

### 1 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mfumo wa e-Office

- Taasisi zote zilizoshiriki zilikuwa zimetekeleza mfumo wa e-Office.
- Miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) ilirahisisha utekelezaji wa mfumo.
- Mfumo umeboresha kwa kiasi kikubwa usimamizi wa taarifa na mawasiliano ya ofisi.

### 2 Manufaa Makuu Yaliyopatikana

Mfumo wa e-Office umewezesha:

- Kuongezeka kwa ufanisi katika usindikaji wa barua.
- Kupunguza matumizi ya nyaraka za karatasi.
- Kuimarisha usalama wa kumbukumbu na uwajibikaji.
- Kurahisisha upatikanaji na ufuatiliaji wa nyaraka.
- Kuongeza uwezo wa kuhifadhi taarifa.
- Kuboresha utoaji wa huduma na maamuzi ya kiutendaji.

### 3 Uwezo wa Taasisi

- Uwezo wa taasisi ulitofautiana kutoka wastani hadi kiwango cha juu.
- Taasisi nyingi zilionesha utayari wa kutekeleza mfumo wa e-Office.
- Ubora na upatikanaji wa miundombinu ya TEHAMA uliathiri mafanikio ya utekelezaji.
- Watumiaji wengi walikuwa na uwezo wa msingi wa kutumia mfumo.

### 4 Mitazamo ya Watumishi

- Watumishi wengi walikuwa na mtazamo chanya kuhusu mfumo.
- Mfumo ulionekana kuwa rahisi kutumia na wenye manufaa.
- Watumishi wengi walionesha kujiamini katika matumizi ya mfumo.
- Baadhi ya watumiaji walikosa ruhusa na haki stahiki za matumizi ya mfumo.

## CHANGAMOTO KUU ZILIZOBAINIKA

- Uhaba wa rasilimali fedha.
- Upinzani dhidi ya mabadiliko ya kiutendaji.
- Upungufu wa ujuzi wa kiteknolojia kwa baadhi ya watumiaji.
- Mapungufu katika usanifu wa mfumo.
- Changamoto za upatikanaji wa intaneti ya uhakika.
- Uhaba wa vifaa vya TEHAMA na msaada wa kitaalamu.
- Tofauti za miundombinu ya TEHAMA kati ya taasisi.

## MAPENDEKEZO MUHIMU

### KWA SERIKALI

- Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya TEHAMA.
- Kupanua upatikanaji wa intaneti yenye uhakika.
- Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mifumo ya e-Office.

### KWA TAASISI SA UMMA

- Kuandaa na kutekeleza sera na miongozo ya matumizi ya e-Office.
- Kuimarisha uongozi na usimamizi wa mabadiliko ya kidijitali.
- Kutenga rasilimali watu na fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa mfumo.

### KWA RAMD NA eGA (WASIMAMIZI NA WAENDELEZAJI WA MFUMO)

- Kuboresha utendaji na usalama wa mifumo ya TEHAMA.
- Kuweka viwango vya pamoja vya miundombinu na mifumo ya TEHAMA.
- Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa mifumo.
- Kuhakikisha uzingatiaji wa sera, viwango, na miongozo ya TEHAMA ya Serikali.

### KWA WATUMISHI

- Kushiriki katika mafunzo endelevu ya TEHAMA.
- Kuongeza ujuzi wa kidijitali na uwezo wa kutumia mifumo ya kielektroniki.
- Kujenga mtazamo chanya kuhusu mabadiliko ya kidijitali.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

# CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)

## MUHTASARI WA UTAFITI (FACT SHEET)

### KAMPASI YA DAR ES SALAAM

# CHANGAMOTO ZA UONGOZI KATIKA KUIMARISHA UTENDAJI WA TAASISI NDANI YA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA: MASUALA MUHIMU NA MWELEKEO WA BAADAYE

TIMU YA WATAFITI: Ausi Nchimbi | Ernest Mabonesho | Hamisi Amani | Musa Ligembe

## LENGO KUU LA UTAFITI

Kuchunguza changamoto kuu za kiuongozi zinazowakabili viongozi katika utumishi wa umma na namna zinavyoathiri utendaji wa taasisi nchini Tanzania.

### Malengo Mahususi ya Utafiti

1. Kuchunguza changamoto zinazohusiana na ujenzi wa motisha kwa watumishi katika utumishi wa umma.
2. Kubaini changamoto zinazojitokeza katika usimamizi wa vipaji na rasilimali watu wenye uwezo mkubwa.
3. Kutathmini uwezo wa viongozi katika kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya haraka yanayotokea katika sekta ya umma.

## MBINU ZA UTAFITI

### Muundo wa Utafiti
- Utafiti wa Kimaelezo wa Kijamii (Qualitative Research Design)

### Misingi ya Kinadharia
- Nadharia ya Uongozi wa Mabadiliko (Transformational Leadership Theory)
- Nadharia ya Usimamizi Mpya wa Umma (New Public Management Theory)

### Mbinu za Ukusanyaji Data
- Mahojiano yenye mwongozo wa maswali huria na nusu-fungamani (Semi-Structured Interviews)

### Washiriki wa Utafiti
Jumla ya viongozi 43 kutoka:
- Wizara
- Sekretarieti za Mikoa
- Wakala za Serikali
- Mamlaka za Serikali za Mitaa

## ATHARI KWA UTENDAJI WA TAASISI

Changamoto hizi husababisha:
- Kupungua kwa tija ya watumishi.
- Kudhoofika kwa ufanisi wa taasisi.
- Kuchelewa kwa utoaji wa huduma kwa wananchi.
- Kupungua kwa imani ya wananchi kwa taasisi za umma.
- Utekelezaji hafifu wa sera, mipango na mageuzi.
- Kupungua kwa ubunifu na ujifunzaji ndani ya taasisi.

## MATOKEO MAKUU YA UTAFITI

### 1 Changamoto za ujenzi wa Motisha kwa Watumishi
- Motisha kwa kiasi kikubwa hutafsiriwa kama malipo ya fedha pekee.
- Kutokuwepo kwa mifumo madhubuti ya kutambua na kuthamini mchango wa watumishi.
- Uwepo wa fursa chache za maendeleo ya kitaaluma na kiutendaji.
- Kushuka kwa ari ya kazi na ushiriki wa watumishi katika shughuli za taasisi.

### 2 Changamoto za Usimamizi wa Vipaji na watumishi wenye uwezo Mkubwa
- Watumishi wenye vipaji na uwezo mkubwa mara nyingi huonekana kama tishio badala ya rasilimali muhimu.
- Mifumo dhaifu ya ulezi, ushauri na ukuzaji wa vipaji.
- Upendeleo katika maamuzi ya kupandisha vyeo na kutoa fursa za maendeleo.
- Udhaifu katika mipango ya urithishwaji wa majukumu na ukuzaji wa viongozi wa baadaye.

### 3 Changamoto za Uwezo wa Kukabiliana na Mabadiliko na Ustahimilivu
- Mabadiliko ya mara kwa mara ya viongozi huathiri mwendelezo wa shughuli za taasisi.
- Uwezo mdogo wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia na sera zinazobadilika kwa kasi.
- Upungufu wa rasilimali unaozuia ubunifu na maboresho ya kiutendaji.
- Ustahimilivu mdogo wa taasisi wakati wa migogoro na vipindi cha mageuzi na mabadiliko.

## MAPENDEKEZO MUHIMU

- Kukuza na kuimarisha uongozi wa mabadiliko (Transformative Leadership) katika taasisi zote za umma.
- Kuimarisha mifumo ya kutambua, kuthamini na kuhamasisha watumishi.
- Kuanzisha na kuendeleza programu rasmi za ulezi, ushauri na ukuzaji wa vipaji.
- Kuhakikisha ajira na upandishaji vyeo vinazingatia sifa, uwezo na utendaji.
- Kuimarisha mafunzo ya viongozi kuhusu uwezo wa kukabiliana na mabadiliko na kujenga ustahimilivu.
- Kujenga utamaduni wa taasisi unaohamasisha ubunifu, ujifunzaji na maboresho endelevu.
- Kuimarisha mifumo ya mwendelezo wa uongozi ili kuhakikisha taasisi zinaendelea kufanya kazi kwa ufanisi licha ya mabadiliko ya viongozi.

# MUHTASARI WA UTAFITI (FACT SHEET)

## KAMPASI YA TABORA

# MATUMIZI YA MFUMO WA UNUNUZI WA UMMA KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI (NeST) NA UTEKELEZAJI WA MFUMO WA FORCE ACCOUNT KATIKA MIRADI YA UJENZI NCHINI TANZANIA

TIMU YA WATAFITI: Richard Manase • Athanas Garaba • Fadhili Mtinda • Emmanuel Mung'onya
Michael Mgongo • Brevius Rudovick

## LENGO KUU LA UTAFITI

Kuchunguza kiwango cha matumizi ya mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya kielektroniki (NeST) na namna Mfumo wa Force Account unavyotumika katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi nchini Tanzania.

### Malengo Mahususi ya Utafiti

1. Kuchunguza kiwango cha matumizi ya mfumo wa NeST nchini Tanzania.
2. Kutathmini matumizi ya Mfumo wa Force Account katika mazingira ya ununuzi wa kielektroniki.
3. Kubaini manufaa yanayotokana na matumizi ya NeST katika utekelezaji wa miradi ya Force Account.
4. Kuchunguza changamoto zinazoathiri utekelezaji wa miradi ya Force Account kupitia mfumo wa NeST.
5. Kubaini changamoto zinazoathiri utekelezaji wa mfumo wa e-Office.

## MBINU ZA UTAFITI

**Muundo wa Utafiti:**
Utafiti wa Kifani (Case Study Design)

**Eneo la Utafiti:**
Mamlaka 18 za Serikali za Mitaa kutoka mikoa sita:
- Kigoma (Halmashauri ya Uvinza, Kasulu, na Buhigwe)
- Tabora (Manispaa ya Tabora Mjini, Halimashauri ya Urambo na Kaliua)
- Shinyanga (Manispaa ya Kahama, Shinyanga na Halimashauri ya Kishapu)
- Geita ( Halimashauri ya Mji Geita, Halimashauri ya Chato na Bukombe)
- Morogoro (Manispaa ya Morogoro, Halimashauri ya Gairo na Mvomero)
- Singida (Manispaa ya Singida, Halimashauri ya Itigi na Manyoni)

**Ukubwa wa Sampuli:**
Washiriki 147

**Washiriki wa Utafiti:**
- Maafisa Ununuzi na Ugavi
- Wahandisi
- Wakuu wa Shule za Sekondari
- Wajumbe wa Kamati za Force Account
- Maafisa Elimu
- Maafisa Uchukuzi

**Mbinu za Ukusanyaji Data:**
- Mahojiano (Interviews)
- Hojaji (Questionnaire)

## MATOKEO MAKUU YA UTAFITI

### 1 Hali ya Matumizi ya Mfumo wa NeST
- Mfumo wa NeST unatumika kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania.
- Umeongeza uwazi na uwajibikaji katika manunuzi ya umma.
- Umeongeza ushindani katika mchakato wa zabuni.
- Umechangia kupunguza mianya ya rushwa.
- Umeboresha usimamizi wa nyaraka za manunuzi.

### 2 Umuhimu wa Mfumo wa Force Account
- Mfumo wa Force Account bado una umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma.
- Unatoa fursa za ajira kwa wananchi wa maeneo husika.
- Unaongeza ushiriki wa jamii katika miradi ya maendeleo.
- Unawezesha utekelezaji wa miradi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mbali.
- Unasaidia kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi.

### 3 Manufaa ya Kuunganisha NeST na Force Account
- Kuboresha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha.
- Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za miradi.
- Kuongeza uwazi katika utekelezaji wa miradi.
- Kuimarisha uwajibikaji.
- Kuboresha usimamizi wa shughuli za manunuzi.
- Kuongeza thamani ya fedha katika miradi ya umma.

## CHANGAMOTO KUU ZILIZOBAINIKA

### Changamoto za Kiteknolojia
- Mfumo kuwa mgumu kwa baadhi ya watumiaji.
- Lugha na istilahi za manunuzi kuwa ngumu kwa wasio wataalamu.
- Kukosekana kwa programu maalumu za kompyuta za mezani.
- Muunganiko hafifu kati ya NeST na mifumo mingine ya serikali kama MUSE.

### Changamoto za Miundombinu
- Changamoto za upatikanaji wa intaneti hasa maeneo ya vijijini.
- Miundombinu duni ya TEHAMA.
- Kutegemea zaidi simu za mkononi na vishikwambi (kwa ngazi za chini mfano Zahanati na Shule-NeST-PE) kuliko kompyuta ambayo inatumika kwa ngazi ya Halimashauri tu.

### Changamoto za Uwezo na Ujuzi
- Upungufu wa wataalamu wenye ujuzi wa kutosha.
- Mafunzo yasiyotosheleza kwa watumiaji.
- Uelewa mdogo wa taratibu za ununuzi wa kielektroniki.

### Changamoto za Sera na Kanuni
- Kutokuwepo kwa mwongozo wa kutosha wa sera.
- Changamoto zinazohusiana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa wakandarasi wadogo.

### Changamoto za Force Account
- Kutolipwa kwa baadhi ya wajumbe wa kamati wa Force Account
- Udhibiti dhaifu wa ubora wa kazi.
- Gharama zilizofichika katika utekelezaji wa miradi.
- Mapungufu ya uwajibikaji wakati wa utekelezaji.

## MAPENDEKEZO MUHIMU

### Kwa Serikali
- Kuimarisha miundombinu ya kidijitali nchini kote.
- Kuboresha upatikanaji wa huduma za intaneti hasa maeneo ya vijijini.
- Kufanyia mapitio sera na kanuni zinazowaathiri wakandarasi wadogo.
- Kuimarisha muunganiko wa mifumo ya kidijitali ya serikali.

### Kwa PPRA na Mamlaka za Ununuzi
- Kurahisisha taratibu na lugha zinazotumika katika mfumo wa NeST.
- Kuboresha urafiki wa mfumo kwa watumiaji.
- Kuimarisha mwongozo wa utekelezaji wa Force Account.

### Kwa Serikali za Mitaa
- Kutoa mafunzo endelevu kwa wadau wa manunuzi.
- Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.
- Kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na uwajibikaji.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
NA UTAWALA BORA

CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)

# MUHTASARI WA UTAFITI (FACT SHEET)

## KAMPASI YA TANGA

# CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO (E-GOVERNMENT) KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA NDANI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (LGAs) NCHINI TANZANIA: UTAFITI WA MAMLAKA TEULE ZA SERIKALI ZA MITAA

**TIMU YA WATAFITI:** Andrew Msagamas • Yuda Kyara • Zawadi Radhid • Josephine Ngonyani • Henry Godda • Grace Mushi

## MAENEO YA UTAFITI

- Halmashauri ya Jiji la Tanga
- Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga
- Halmashauri ya Manispaa ya Moshi
- Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga
- Halmashauri ya Wilaya ya Same

**Mikoa Iliyohusika**
- Tanga
- Kilimanjaro

## LENGO KUU LA UTAFITI

Kuchunguza changamoto zinazokwamisha matumizi ya Serikali Mtandao (e-Government) na athari zake katika utoaji wa huduma ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini Tanzania.

### Malengo Mahususi ya Utafiti

1. Kutathmini ufanisi wa miundombinu ya TEHAMA inayosaidia mifumo ya Serikali Mtandao.
2. Kuchunguza uwezo wa watumishi katika matumizi ya mifumo ya Serikali Mtandao.
3. Kutathmini mtazamo na kiwango cha imani ya wadau kuhusu huduma za Serikali Mtandao.
4. Kubaini changamoto zinazoathiri utekelezaji wenye mafanikio wa mipango ya Serikali

## MATOKEO MAKUU YA UTAFITI

### 1 Miundombinu ya Tehama
- Miundombinu ya TEHAMA ipo katika Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa.
- Mifumo ya kidijitali kama GePG, GAMIS, NeST, PEPMIS, PLANREP na LGRCIS inatumika.
- Miundombinu bado haitoshi katika maeneo mengi ya vijijini.
- Changamoto ya mtandao hafifu wa intaneti inaathiri utoaji wa huduma.

### 2 Uwezo wa Watumishi
- Watumishi wengi wana ujuzi wa msingi wa matumizi ya teknolojia za kidijitali.
- Watumishi wengi wanafahamu matumizi ya mifumo mikuu ya Serikali Mtandao.
- Ujuzi wa juu wa TEHAMA na usimamizi wa mifumo bado ni mdogo.

Kuna haja ya kuendelea kuwajengea watumishi uwezo mara kwa mara.

### 3 Mtazamo na Imani ya Wadau
- Wananchi kwa ujumla wana imani na huduma za Serikali Mtandao.
- Matumizi ya mifumo ya malipo kwa njia ya mtandao yanaendelea kukubalika.
- Wadau wanaona Serikali Mtandao imeongeza uwazi na urahisi wa kupata huduma.
- Bado kuna wasiwasi kuhusu utegemevu wa mifumo, faragha na usalama wa taarifa.

## MBINU ZA UTAFITI

**Muundo wa Utafiti**
Utafiti ulitumia muundo wa maelezo unaochanganya mbinu za kiasi na ubora (Mixed Methods).

**Ukubwa wa Sampuli**
Wahojiwa 204

**Mbinu za Ukusanyaji wa Data**
- Dodoso
- Mahojiano
- Mapitio ya Nyaraka

## CHANGAMOTO KUU ZILIZOBAINIKA

**Changamoto za Miundombinu**
- Upungufu wa vifaa vya TEHAMA
- Huduma hafifu ya intaneti
- Umeme usioaminika
- Mtandao kutofika katika baadhi ya maeneo ya vijijini

**Changamoto za Rasilimali Watu**
- Upungufu wa ujuzi wa TEHAMA
- Fursa chache za mafunzo
- Upinzani dhidi ya mabadiliko ya kiteknolojia

**Changamoto za Kitaasisi**
- Mifumo kutofanya kazi kwa pamoja
- Ushirikiano hafifu wa mifumo mbalimbali
- Uratibu mdogo wa sera na miongozo

**Changamoto za Kifedha**
- Bajeti ndogo za TEHAMA
- Upungufu wa fedha za matengenezo na maboresho ya mifumo

**Changamoto za Usalama wa Taarifa**
- Hatari za mashambulizi ya mtandao
- Hofu kuhusu faragha ya taarifa
- Uelewa mdogo wa usalama wa kidijitali

**Changamoto za Upatikanaji wa Huduma**
- Pengo la kidijitali kati ya maeneo ya mijini na vijijini
- Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu huduma za kidijitali
- Upatikanaji mdogo wa vifaa vya kidijitali

## MAPENDEKEZO MUHIMU

**Kwa Serikali**
- Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya TEHAMA.
- Kupanua huduma za intaneti kwa maeneo ya vijijini.
- Kuimarisha mifumo ya usalama wa mtandao.
- Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya mabadiliko ya kidijitali.

**Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**
- Kuimarisha muunganiko na ushirikiano wa mifumo mbalimbali.
- Kuboresha usimamizi wa TEHAMA.
- Kuanzisha programu endelevu za mafunzo kwa watumishi.

**Kwa Watumishi wa Umma**
- Kuongeza ujuzi wa hali ya juu wa kidijitali.
- Kukubali na kutumia teknolojia katika utoaji wa huduma.
- Kushiriki mara kwa mara katika mafunzo ya kujengewa uwezo.

**Kwa Jamii**
- Kukuza uelewa wa matumizi ya teknolojia za kidijitali.
- Kuhamasisha matumizi ya huduma za serikali zinazopatikana mtandaoni.
- Kujenga imani kwa wananchi kuhusu mifumo ya Serikali Mtandao.

**Changamoto za Upatikanaji wa Huduma**
- Pengo la kidijitali kati ya maeneo ya mijini na vijijini
- Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu huduma za kidijitali
- Upatikanaji mdogo wa vifaa vya kidijitali

CHUO CHA UTUMISHI TANZANIA (TPSC)
S.L.P 2574, Dar Es Salaam,
TANZANIA

+255 22 286 0370-5 | info@tpsc.go.tz | https://www.tpsc.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
NA UTAWALA BORA

CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)

# MUHTASARI WA UTAFITI (FACT SHEET)

## KAMPASI YA MBEYA

# UFANISI WA PROGRAMU ZA MAFUNZO YA KUJENGA UWEZO KATIKA KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA KATIKA TAASISI ZA UMMA TANZANIA

TIMU YA WATAFITI: Saidy Nzagamba | Livin Leon | Said Hassan | Boniface Abel | Veronica Kasake

## LENGO KUU LA UTAFITI

Kutathmini ufanisi wa programu za mafunzo ya kujenga uwezo (capacity-building training programs) katika kuboresha utoaji wa huduma ndani ya taasisi za umma nchini Tanzania.

### Malengo Mahususi

1. Kutathmini umuhimu na ubora wa programu za mafunzo.
2. Kuchunguza kiwango cha maarifa na ujuzi unaopatikana baada ya mafunzo.
3. Kutathmini matumizi ya maarifa na ujuzi uliopatikana mahali pa kazi.
4. Kubaini mchango wa mafunzo katika kuboresha utoaji wa huduma.
5. Kutambua changamoto zinazoathiri ufanisi wa programu za mafunzo.

## MBINU ZA UTAFITI

### Muundo wa Utafiti

Muundo Sambamba wa Mchanganyiko wa Mbinu za Utafiti (Convergent Parallel Mixed Methods Design) ili

- kuchunguza kwa kina namna mafunzo ya kujenga uwezo yanavyotekelezwa,
- kubaini jinsi yanavyochangia katika kuongeza umahiri wa watumishi, na
- kubaini namna mafunzo yanavyoathiri utoaji wa huduma katika mazingira halisi ya taasisi za umma.

### Washiriki

Wahojiwa 178 kutoka taasisi mbalimbali za umma:

### Eneo la Utafiti na Taasisi Zilizohusishwa

- Wizara za Serikali Kuu
- Sekretarieti za Mikoa
- Mamlaka za Serikali za Mitaa /Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma

### Mbinu za Ukusanyaji Data

- Dodoso
- Mahojiano
- Mapitio ya Nyaraka
- Uangalizi

## MATOKEO MAKUU YA UTAFITI

### 1. Umuhimu na Ubora wa Mafunzo

- Programu nyingi za mafunzo zilionekana kuendana na mahitaji ya kazi.
- Maudhui ya mafunzo yalikuwa ya kisasa na yenye manufaa kwa utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- Maeneo yanayohitaji kuboreshwa ni tathmini ya mahitaji ya mafunzo, ufuatiliaji na msaada baada ya mafunzo.

### 2. Maarifa na Ujuzi Uliopatikana

- Washiriki waliripoti ongezeko kubwa la maarifa na ujuzi baada ya kushiriki mafunzo.
- Mafunzo yaliboresha uwezo wa kiufundi, kiutawala na uhusiano wa kijamii mahali pa kazi.

### 3. Matumizi ya Mafunzo Mahali pa Kazi

- Wengi wa washiriki walitumia maarifa na ujuzi waliopata katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.
- Msaada kutoka kwa wasimamizi na upatikanaji wa rasilimali uliathiri kiwango cha matumizi ya ujuzi huo.
- Baadhi ya taasisi ziliripoti kuwepo kwa fursa chache za kutumia ujuzi uliopatikana.

### 4. Athari za Mafunzo katika Utoaji wa Huduma

- Mafunzo yalichangia kuongeza ufanisi, usahihi na kasi ya utoaji wa huduma.
- Yaliboresha kuridhika kwa wananchi na kupunguza malalamiko.
- Yalikuwa na mchango chanya katika ushirikiano kazini na kuongeza tija ya wafanyakazi.
- Yalisaidia kuongeza morali ya ufanyaji wa kazi kwa watumishi katika maeneo yao ya kazi

## CHANGAMOTO KUU ZILIZOBAINIKA

- Bajeti ndogo za mafunzo.
- Kutofanyika mara kwa mara kwa tathmini za mahitaji ya mafunzo.
- Ufuatiliaji na tathmini hafifu baada ya mafunzo.
- Kuhama kwa watumishi waliopatiwa mafunzo.
- Mzigo mkubwa wa kazi unaozuia matumizi ya ujuzi uliopatikana.
- Baadhi ya watumishi kutozingatia utekelezaji wa mafunzo husika katika maeneo yao ya kazi.

## MAPENDEKEZO MUHIMU

### KWA SERIKALI

- Kuongeza uwekezaji katika programu za kujenga uwezo.
- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na viwango vya kitaifa vya mafunzo.
- Kuhakikisha tathmini na ufuatiliaji wa mahitaji ya mafunzo unafanyika mara kwa mara.

### KWA TAASISI ZA UMMA

- Kuoanisha mafunzo na malengo ya taasisi.
- Kuhakikisha uwepo wa ufuatiliaji, ushauri elekezi na msaada kazini baada ya mafunzo.
- Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya mafunzo na matumizi ya ujuzi unaopatikana.

### KWA WATOA MAFUNZO

- Kubuni mafunzo yenye kuzingatia vitendo, ushirikishwaji na matokeo.
- Kutumia mbinu na teknolojia za kisasa katika utoaji wa mafunzo.
- Kufanya tathmini ya athari za mafunzo baada ya utekelezaji wake.
- Kujua mahitaji halisia ya mafunzo kwa watumishi kabla ya kuyaandaa.(Yenye tija kwa mahitaji ya taasisi)

### KWA WATUMISHI

- Kushiriki kikamilifu katika programu za mafunzo.
- Kutumia maarifa na ujuzi walioupata katika utekelezaji wa majukumu yao.
- Kushirikishana maarifa na wenzao na kuendeleza utamaduni wa kujifunza kazini.
- Kuendelea kujifunza na kujiboresha kitaaluma hata baada ya mafunzo rasmi kumalizika.